

Kuvuna

Huchukua miezi 3 kabla ya kuvunwa baada ya thuluthi tatu kufunguka.

- Kata kwa kutumia kisu kikali kisha ondoa majani ya chini ya mhimili na uyaweke katika mtungi wa maji wa plastiki kwa dawa ya kuhifadhi kama vile *Florissant* na maua yawekwe kwenye kivuli ili kuzuia joto jingi.

Mavuno na faida

- Mazoa ni miti 120-180 kwa kila mita moja na kati ya 280,000-320,000 kwa kila ekari.
- Faidi kwa kila mita 100 mraba ni Shilingi 7,100.28.
- Faida kwa kila ekari ni Shilingi 712,800.00.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Muriithi, A M

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI Thika

S.L.P. 220-01000, Thika

Simu: 020-2055038

Baruapepe: karithika@africaonline.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 28 / 2008

Shilingi 20 za Kenya

Ukuzaji wa maua ya Ammi



Utangulizi

Ua la *Ammi* lina rangi ya mchanganyiko wa manjano na weupe. Lina manukato kidogo na hukuzwa kwa kutumia mbegu. Ni mmea wa msimu mfupi na hukubaliana na aina kadha za upaliliaji na kukuzwa kwake hakuna gharama ya juu.

Aina za maua ya *Ammi*

Aina zinazokuzwa Kenya hasa ni:

- *Ammi majus*: ua hili huwa na kichwa cheupe, na upana wa sentimita 15.
- *Ammi visinaga*: ua hili huwa fupi kuliko *Ammi majus* na lina rangi ya mchanganyiko wa weupe na kijani.

Mahitaji ya ukuzaji

- *Ammi* hukubaliana vyema na aina kadhaa za michanga zenye mbolea ya hali ya juu na ambayo inaweza kuhifadhi unyevu unaohitajika.

Matayarisho ya kitanda cha kupandia

- Chimbua mchanga kwa undani.
- Tia mbolea nzuri katika mchanga, kiasi cha kilogramu 10 kwa mita jumla.

- Tayarisha vitanda vya kupandia vya upana wa mita moja na urefu ufaao, na kinjia cha sentimita 50.
- Tayarisha mitaro isiyo ya ndani sana huku ukiacha nafasi ya sentimita 15 katikati ya mitaro.

Kupanda

- Nyunyizia maji kwenye kitanda siku moja kabla ya kupanda na uloweshe mchanga ukipanda.
- Panda mbegu kwenye ardhi moja kwa moja kwa kutoboa mashimo juu ya mitaro na kutia gramu 30 kwa kila mita mia 100 jumla.
- Funikia vitanda na majani ili kuzuia kupoteza unyevu muda tu baada ya kupanda.
- Bada ya kuota, kata mimea-chipukizi uache mimea 30 kwa kila mita jumla.

Kunyunyizia Maji

- Ili kuhakikisha mimea imekua vyema, nyunyizia maji kutoka juu hadi wakati wa maua kuchipuka. Baada ya maua kuchipuka, tumia kinyunyizio cha matone (drip) au aina zingine.

Kupalilia

Kupalilia kunafaa kufanywa kwekwe zitokeapo ili kudumisha shamba safi.

Mbolea ya juu

- Tia *Nitrogen* kiasi cha gramu 50 kwa mita jumla *NPK 17: 17: 17* mwezi mmoja baada ya kupanda.
- Kiasi cha *Nitrogen* kilichopita kiwango husababisha matawi manyonge, maua ya kiwango cha chini na mazao duni.
- Weka molea ya matawi ya *Potassium Nitrate* kila baada ya wiki mbilil kuanzia mwezi wa pili ili kuimarisha ubora wa maua.

Usaidizi

- Matawi ya *Ammi* ni dhaifu na huinama kabla ya kukomaa na yanahitaji kushikiliwa.
- Vifaa vinavyotumiwa kushikilia ni kama vile neti, waya na miti ya mianzi ikitiwa mara tu baada kupanda.
- Vuta waya wa kwanza wa kushikilia katikati ya mitaro urefu wa sentimita 30 kutoka chini.
- Vijiti vya mianzi vinafaa kuwekelewa juu ya kitanda, kati ya mimea.
- Weka waya zilizopindwa juu na chini ya miti ya mianzi.